BU African Studies Center LANGUAGE PROGRAM, 232 BAY STATE ROAD, BOSTON, MA 02215
www.bu.edu/Africa/alp
africa@bu.edu
617.353.3673

**Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo: Mazoezi**

**Zoezi la 1:** Toa maana ya maneno haya

i) Kufaa
ii) Wasiwasi
iii) Kwema
iv) Simu
v) Kuokota
vi) Kuiba
vii) Uwizi
viii) Kusingizia
ix) Kunyanyasa
x) Kuamua

**Zoezi la 2: Tungia Sentensi maneno katika zoezi la 2 kisha utafsiri**

**Zoezi la 3: Jibu maswali haya**

i) Siku ya kwanza kijana alileta nini? Alisema ametoa wapi?
ii) Alileta nini siku ya pili? Alitoa maelezo gani?
iii) Na ya tatu je? Alisemaje kuhusu kitu hicho?
iv) Baba ya kijana alisema nini kila mara mtoto aliporudi na kitu?
v) Kama wewe ungekuwa mzazi wa mtoto kama huyu, ungemwambia nini akija na vitunyumbani?

**Zoezi la 4: Jibu kweli au Si kweli**

i) Watoto wadogo wanaweza kuwa wezi
ii) Baba yule alimkanya kijana wake kila siku
iii) Mama alimnunulia mtoto wake mpira
iv) Kijana hakuiba baiskeli
v) Kijana alipelekwa polisi

© Boston University

vi) Katika kisa hiki Baba ndiye mwenye makosa

vii) Mtoto hakuwa na kosa lolote

viii) Majirani walijua kijana yule alikuwa na tabia mbaya ya uwizi

ix) Tusipowakataza watoto mapema wanaweza kuzoea kufanya vitu vibaya

x) Watoto wakilelewa vibaya wanaweza kuwa wazuri

**Zoezi la 5: Kuelezea maana**

Elezea maana ya methali hii "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" kama
Ilivyotumika katika hadithi hii.

**Zoezi la 6: Kuandika muhtasari**

Andika Muhtasari wa igizo hili kama unamwadithia mtu mwingine.

**Zoezi la 7: Kulinganisha na kutofautisha**

Tofautisha methali hizi, "mtoto akililia wembe mpe" na "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo"

**Zoezi la 8: Jibu swali hili**

Taja methali au msemo wa Kiingereza unayofanana na methali hii
Unaweza kuelezea methali hiyo hutumikaje?

**Zoezi la 9: Jibu Swali hili**

Andika kisa kifupi kuelezea methali "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo"

**Zoezi la 10: Jibu swali hili**

Jaribu kuigiza methali hii ili kufanya mazoezi